**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA TANGA

# AGIZO LA UNUNUZI WA KANDARASI UKARABATI WA CHUMBA CHA ICU HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA

KATI YA

KATIBU TAWALA MKOA
S. L. P 5095
TANGA

NA

MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES COMPANY LTD
S.L.P 1098
TANGA

**ME/007/2021-22/RRHMTAN/W/10**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA TANGA

## AGIZO LA UNUNUZI WA KANDARASI UKARABATI WA CHUMBA CHA ICU HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA

KATI YA

KATIBU TAWALA MKOA
S. L. P 5095
TANGA

NA

MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES COMPANY LTD
S.L.P 1098
TANGA

**ME/007/2021-22/RRHMTAN/W/10**

Kwa **Mashani Construction and General**
**Supplies Company Ltd**
**S.L.P 1098, Tanga**

Kotesheni yako yenye kumbukumbu Na. **ME/007/2021-22/RRHTAN/W/10** ya tarehe 31/12/2021 imekubaliwa na unatakiwa kutekeleza Kandarasi ya Ukarabati kama ilivyoelezwa katika Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ulioambatishwa kulingana na masharti yaliyomo katika Agizo la Ununuzi *(ALU)*. Agizo hili limetolewa kulingana na MMM na MJM ya ALU, isipokuwa pale ambapo imebadilishwa na masharti yaliyoainishwa hapo chini.

**VIGEZO NA MASHARTI YA AGIZO LA UNUNUZI:**

1. **Gharama za Mkataba:** Gharama za mkataba ni **Tzs 5,350,000 (Millioni Tano, Laki Tatu na Hamsini Elfu** *[inayojumuisha VAT]*;

2. **Muda wa kutekeleza kazi:** Kazi itatekelezwa ndani ya **siku 30** kuanzia tarehe ya Agizo la Ununuzi;

3. **Kipindi cha Matazamio ya Marekebisho:** Kipindi cha matazamio ya Marekebisho kimeaninishwa katika sehemu ya MMM ya Agizo hii;

4. **Eneo la Kazi:** Kandarasi hii itatekelezwa Hospitali ya Rufaa Mkoa Tanga katika Jengo la ICU kama ilivyotafsiriwa katika michoro;

5. **Mawasiliano:** Notisi, maulizo na nyaraka kutoka kwa Mkandarasi zitatumwa kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa Tanga, S.L.P 452, Tanga;

6. **Malipo kwa Mkandarasi:**

   Malipo yatafanywa baada ya utekelezaji wa kazi au sehemu ya kazi ndani ya siku kumi na nne baada ya tarehe ya kuidhinishwa kwa Hati ya Kukubali kazi. Nyaraka zifuatazo ziwasilishwe ili malipo yafanyike:

   - Ankara halisi ya malipo na nakala mbili ya ankara hiyo;
   - Maombi ya Kukamilika kwa Sehemu ya Kaz iliyokubaliwa;
   - Hati ya Ukamilishaji wa kazi kilichokubaliwa na kusainiwa na Mhusika au Kamati ya Ukaguzi wa kazi;
   - Ankara ya Kielektroniki; na

7. Nyaraka zifuatazo zinaunda sehemu ya mkataba huu:

- Agizo la Ununuzi (LPO);
- Barua ya Tuzo ya Zabuni;
- Muhtasari wa Kikao cha Majadiliano (kama yapo)
- Fomu ya kuwasilisha Kotesheni;
- Masharti Maalum ya Mkataba;
- Masharti ya Jumla ya Mkataba;
- Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi
- Vigezo Msawazo wa kiufundi, Michoro, Ramani, Vipimo Sanifu;
- Nyaraka nyinginezo.

8. Mkataba huu umefanyika kutiwa sahihi leo tarehe **04 Mwezi 01 Mwaka, 2022**.

| **MWAJIRI:** | **MKANDARASI/FUNDI UJENZI:** |
|---|---|
| Saini: ........................ | Saini: ........................ |
| Jina: PILI H. MNYEMA | Jina: SHABANI ALLY MRINDOKO |
| Cheo: RAS | Cheo: MANAGING DIRECTOR (MD) |
| Tarehe: 04/1/2022 | Tarehe: 4/01/2022 |
| KATIBU TAWALA WA MKOA TANGA | MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES CO. LTD P.O. Box 1098 TANGA TANZANIA |
| **Mbele ya;** | **Mbele ya;** |
| Saini: ........................ | Saini: ........................ |
| Jina: ABDI D. MSOTI | Jina: ABUBAKARI RAMADHANI |
| Cheo: AFISA SHERIA | Cheo: PROJECT MANAGER |
| Tarehe: 29/12/2021. | Tarehe: 4/01/2022 |

MASHANI CONSTRUCTION AND

GENERAL SUPPLIES CO. LTD

S.L.P 1098

**TANGA**

03/01/2022

MGANGA MFAWIDHI,

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TANGA,

S.L.P 452,

**TANGA**

YAH: **KUKUBALI KUFANYA KAZI YA UFUNDI WA UKARABATI WA CHUMBA CHA ICU (ME/007/2021-22/RRHTAN/W/10)**

Ndugu rejea somo tajwa hapo juu,

Nakiri kupokea barua yako yenye Kumb no. Ref. NO: **RM/F.20/13VOLV/11** ya tarehe **03/01/2022** ya kuchaguliwa kazi ya Ukarabati wa Jengo la ICU.

Napenda kutoa shukrani zangu kwa Kamati iliyonichagua kufanya kazi hiyo ya Ufundi wa Ukrarbati. Nakiri kuwa nitaifanya kazi hiyo kwa wakati na kwa ubora unaohitajika kwa gharama ya Tshs. 5,350,000/=.

Nakuahidi ushirikiano katika kazi hii mpaka itakapokamilika.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

..............................................

**SHABANI ALLY MRINDOKO**

MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES CO. LTD. P.O. Box 1098 TANGA TANZANIA

# MAELEKEZO KWA WAZABUNI

| | |
|---|---|
| 1.0 | Hospitali ya Rufaa Mkoa Tanga inaalika Kotesheni kwa ajili ya Ujenzi wa Chumba cha Upasuaji kama ilivyoainishwa kwenye Vigezo Msawazo vya Kiufundi na Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi. Mzabuni Mshindi anatarajiwa kutekeleza kazi katika eneo la Idara ya dharula (EMD) na kazi inapaswa kukamilika ndani ya **siku 30** baada ya Mkataba kusainiwa. |
| 2.0 | 2.1 Mzabuni anaweza kuwa mtu Binafsi, Kampuni, Ushirika, Taasisi au Shirika la Umma au Kikundi cha watu kilichosajiliwa kisheria au ushirika au ubia baina yao.<br><br>2.2 Mwaliko wa Kotesheni hii ni kwa mzabuni aliepewa mwaliko.<br><br>2.3 Mzabuni atapaswa kutimiza matakwa ya leseni na usajili ya mamlaka za kisheria za Tanzania. Wazabuni wa nje ya nchi hawaruhusiwi kushiriki zabuni hii.<br><br>2.4 Mzabuni hatapaswa kuwa na mgongano wa masilahi. Wazabuni wote watakaogundulika kuwa na mgongano wa masilahi watakosa sifa ya kushiriki zabuni hii.<br><br>2.5 Mzabuni hatastahili kuomba au kushinda zabuni hii iwapo: –<br><br>(a) Mzabuni ametangazwa muflisi;<br>(b) Malipo kwa Mzabuni yamesimamishwa kwa mujibu wa hukumu ya mahakama mbali na hukumu ya kutangaza kufilisika na itokanayo, kwa mujibu wa sheria za nchi, kupoteza kwa ujumla au sehemu haki ya kusimamia na kuondosha mali zake;<br>(c) Michakato ya kisheria imeanzishwa dhidi ya mzabuni inayohusisha agizo la kusimamisha malipo na inayoweza kupelekea, kwa mujibu wa sheria za nchi, kutangawa kufilisika au katika hali nyingine yeyote itakayopelekea kupoteza kwa ujumla au sehemu haki ya |

| | |
|---|---|
| | kusimamia na kuondosha mali;<br>(d) Mzabuni amehukumiwa kwa hukumu ya mwisho, ya kosa lolote linalohusisha maadili ya kitaalamu;<br>(e) Mzabuni amefungiwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 na Kanuni zake za Mwaka 2013 kushiriki katika ununuzi wa umma kwa ajili ya vitendo vya rushwa, kulazimisha, kula njama, udanganyifu au kuzuia, kushinda kuheshimu tamko la dhamana ya zabuni, kukiuka mkataba wa ununuzi, kuwasilisha sifa za uongo katika mchakato wa zabuni au vigezo vingine vitakavyoonekana vinafaa na Mamlaka au kampuni imepatikana na kosa kubwa la udanganyifu wa taarifa zilizohitajika kwa ajili ya ushiriki katika mwaliko wa zabuni.<br>2.6 Mashirika ya Umma au mashirika yanayomilikiwa kati ya Umma na makampuni binafsi yanaweza kushiriki katika zabuni hii, iwapo tu wanajitegemea kisheria na kifedha, kama wanafanya kazi chini ya sheria ya biashara, siyo wakala zinazoitegemea Serikali na wamesajiliwa na bodi au mamlaka husika.<br>2.7 Wazabuni watawasilisha uthibitisho wa sifa zao endelevu kwa kiwango cha kuiridhisha Taasisi Nunuzi, kama Taasisi Nunuzi itakavyowaomba. |
| 3.0 | Mzabuni ataambatisha nyaraka zifuatazo katika Kotesheni yake:<br>(a) Pendekezo lake la bei lililojazwa kikamilifu na kusainiwa kwa mujibu wa Mchanganuo wa Makadirio ya kazi (BoQ);<br>(b) Cheti ya Usajili wa Kampuni/kikundi<br>(c) Leseni halali ya Biashara;<br>(d) Hati Halali Usajili wa VAT (*kama ipo*)<br>(e) Cheti Safi ya Mlipa kodi (Tax Clearance Certificate);<br>(f) Orodha ya mikataba iliyotekelezwa karibuni inayojumuisha majina |

| | |
|---|---|
| | na anuani za Wanunuzi kwa ajili ya uthibitisho;<br>(g) Tamko la Dhamana ya Zabuni;<br>(h) Hati ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria Iliyoidhinishwa (*isipokuwa kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja (sole proprietor);*<br>(i) Fomu ya Uadilifu iliyo katika Sehemu ya Nane iliyojazwa na kusainiwa; |
| 4.0 | Taarifa za Vigezo Msawazo vya Kitaalam na michoro vimeambatishwa katika **Sehemu ya Saba**. |
| 5.0 | Bei ya Zabuni:<br>5.1 Mkataba utakuwa kwa idadi iliyofafanuliwa katika Sehemu ya Pili;<br>5.2 Marekebisho yoyote, kama yatakuwepo, yanaweza kufanyika kwa kubadilisha zabuni ambayo imekwisha wasilishwa muda wowote kabla ya muda wa mwisho wa kuwasilisha zabuni kupitia TANePS. Aidha, marekebisho yanaweza pia kufanyika kwa kukata sehemu husika, kuweka saini ya mtu aliyeidhinishwa, tarehe na kuandika kwa usahihi kabla kuwasilisha nyaraka kupitia TANePS, muda wowote kabla ya muda wa mwisho wa kuwasilisha zabuni.<br>5.3 Ushuru, kodi na ada zote zinazolipwa na Mzabuni chini ya Mkataba zijumuishwe kwenye jumla ya bei.<br>5.4 Vizio vya kima vilivyotajwa na Mzabuni na kukubalika na pande zote za Mkataba havitabadilika katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mkataba<br>5.5 Bei zinapaswa kunukuliwa katika Shilingi ya Tanzania. |
| 6.0 | 5.1 Mzabuni atakamilisha kujaza fomu ya kuwasilisha Kotesheni ambayo imeambatishwa. Fomu hiyo ya kotesheni, itajazwa kikamilifu bila kubadili muundo wake na hakuna fomu mbadala itakayokubaliwa. |

| | |
|---|---|
| | 7.1 Malipo yatafanywa katika Shilingi ya Tanzania. |
| 8.0 | 8.1 Kotesheni itabaki kuwa halali kwa kipindi cha siku 45 baada ya siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni . |
| 9.0 | 9.1 Kotesheni Mbadala *"hazitumiki"*. |
| | 9.2 Kama Kotesheni mbadala zinakubalika, Mzabuni anayetaka kufanya Mabadiliko ya kiufundi kwa mahitaji ya nyaraka za Kotesheni, lazima pia, awasilishe Kotesheni inayozingatia mahitaji ya nyaraka za Kotesheni, ikiwa ni pamoja na ufundi sanifu kama ilivyoonyeshwa kwenye Vigezo Msawazo. Pamoja na kuwasilisha Kotesheni hiyo, Mzabuni atatoa taarifa zote muhimu kwa ajili ya **TN** kukamilisha tathmini ya Kotesheni mbadala iliyotolewa, ikiwa ni pamoja na Vigezo Msawazo, mchanganuo wa bei, pamoja wa masuala mengine yanayohusika. Ni mbadala ya kiufundi tu kama utakuwapo, wa Mzabuni mwenye zabuni yenye bei ndogo iliyokidhi vigezo vya tathmini inayozingatia mahitaji ya msingi ya kiufundi ndiyo itafikiriwa na TN. |
| 10.0 | 10.1 Isipokuwa kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja (sole proprietor), Zabuni itakamilishwa na kusainiwa na mwakilishi aliyeidhinishwa na Mzabuni. Kwa muktadha huu Hati ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria itawasilishwa pamoja na Kotesheni hii. |
| 11.0 | 11.1 Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe kwa **Hospitali ya Rufaa Mkoa Tanga** kupitia TANePS kabla ya **05/01/2022 saa nne asubuhi** ya kuwasilisha Kotesheni. Ufunguzi wa Kotesheni hizo utafanyika kupitia TANePS mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Kotesheni. |
| 12.0 | TN itafanyia tathmini na kulinganisha Zabuni kwa namna ifuatayo: |
| | 12.1 Tathmini ya Awali; ili kutambua ni Zabuni zipi zinakidhi matakwa ya msingi ya nyaraka za Zabuni, kama vile: zilezilizosainiwa kwa usahihi na |

| | |
|---|---|
| | zilizotimiza vigezo na masharti ya Mwaliko wa Zabuni.<br><br>a) Leseni halali ya Biashara;<br><br>b) Cheti ya Usajili wa Kampuni/kikundi<br><br>c) Cheti ya usajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB)<br><br>d) Hati Halali Usajili wa VAT (*kama ipo*)<br><br>e) Cheti Safi ya Mlipa kodi (Tax Clearance Certificate);<br><br>f) Fomu ya kuwasilisha zabuni yenye bei iliyojazwa kikamilifu na kusainiwa ipasavyo sambamba na Jedwali la Mahitaji na Bei;<br><br>g) Tamko la Dhamana ya Zabuni;<br><br>h) Hati Sanifu ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria Iliyoidhinishwa (*isipokuwa kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja (sole proprietor);*<br><br>i) Fomu ya Uadilifu iliyo katika Sehemu ya Nane iliyojazwa na kusainiwa;<br><br>j) Uwezo/utayari wa mzabuni kuendana na muda uliowekwa wa kumaliza kazi<br><br>k) nyaraka nyingine zozote zitakazohitajika [*ongeza nyaraka nyingine*]<br><br>Kama sehemu ya tathmini ya awali, TN itaangalia:<br><br>(a) Orodha ya mikataba iliyotekelezwa karibuni inayojumuisha majina na anuani za taasisi zilizopokea huduma kwa ajili ya uthibitisho;<br><br>(b) Uthibisho wa kimaandishi kwamba Mzabuni alikamilisha mkataba/mikataba inayofanana na huu kwa ufanisi.<br><br>(c) Uwezo wa kifedha; |

| | |
|---|---|
| | (d) [*ingiza vigezo vingine vya muhimu*] ambavyo vinahitajika<br><br>Angalizo: Kukosekana kwa kigezo kimojawapo kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu, au kubadili maneno ya fomu sanifu zilizoambatanishwa kwenye nyaraka hizi kutasababisha mzabuni kuenguliwa kwenye hatua hii ya tathmini ya awali.<br><br>12.2 Zabuni zitakazokidhi matakwa ya Nyaraka za Zabuni zitafanyiwa Tathmini ya Kina kwa;<br><br>(a) Kufanya marekebisho ya makosa ya kihesabu: kama kutakuwa na tofauti ya kimahesabu kati ya kizio cha kima (unit rate) na kiasi (sub-total amount) kilichowasilishwa, basi kizio cha kima kitatumika katika tathimini ya Zabuni na katika Makubaliano ya Mkataba utakaofuata.<br><br>(b) Kufanya marekebisho stahili, kwa ajili ya mabadiliko yanayokubalika, (variations, deviations) au mabadiliko yanayotokana na kutowekwa kwa baadhi ya vipengele;<br><br>(c) Kufanya marekebisho stahili kuakisi punguzo la bei ya tuzo au marekebisho mengine ya bei yaliyotolewa<br><br>12.3 Ulinganishaji wa Kotesheni; Katika kufanya tathmini ya Kotesheni, kamati ya tathmini itaweka kwa kila Kotesheni, bei ya Zabuni iliyofanyiwa tathmini ili kubaini Mzabuni mwenye bei ndogo:<br><br>12.4 Mzabuni atakayeonekana kuwa na bei ndogo baada ya kufanyiwa tathmini, atafanyiwa uhakiki wa uwezo na sifa ili kujiridhisha kwamba ataweza kuingia mkataba na kutekeleza majukumu yake ya mkataba kwa ufanisi. |
| 13.0 | 13.1 TN itatoa tuzo ya mkataba kwa mzabuni ambaye Kotesheni yake imekidhi vigezo vya Kotesheni, na ambayo imewasilisha bei ndogo ya |

| | |
|---|---|
| | Kotesheni baada ya kufanyiwa tathmini. |
| 14.0 | 14.1 TN inayo haki wakati wa kutoa tuzo ya Mkataba kuongeza au kupunguza hadi asilimia kumi na tano (15%)ya idadi ya kazi ambazo zilibainishwa hapo awali katika Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi bila mabadiliko yoyote ya bei ya kima cha kizio kimoja au masharti mengine na hii itaonyeshwa kwenye fomu ya Mkataba. |
| 15.0 | 15.1 Bila ya kuathiri yaliyotajwa hapo juu, TN inayo haki ya kukubali au kukataa Kotesheni yoyote wakati wowote kabla ya kutoa tuzo. |
| 16.0 | 16.1 Kabla ya kutoa tuzo ya Mkataba, TN itatoa Barua ya Kusudio la kutoa Tuzo kwa Wazabuni wote walioshiriki katika zabuni hiyo ikitoa siku saba za kazi kwa Wazabuni hao kuwasilisha malalamiko yoyote (kama yatakuwepo kupitia TANePS. Endapo Mzabuni hataridhika na maamuzi ya TN, anaweza kukata rufaa kwenye Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (PPAA). |
| 17.0 | 17.1 Mzabuni ambaye Kotesheni yake imekubaliwa atajulishwa na TN kuwa amekubaliwa kupewa tuzo ya mkataba kabla ya kwisha kwa kipindi cha uhai wa Kotesheni (Fomu ya mkataba pamoja na masharti yote ya malipo yanapaswa kutolewa kwa Mkandarasi pamoja na huu mwaliko wa kotesheni). |
| 18.0 | 18.1 Mzabuni Mshindi atatakiwa kuwasilisha Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kukamilika kwa masharti ya kabla ya kusaini mkataba baada ya kupokea barua ya tuzo na kabla kusainiwa Mkataba. |
| 19.0 | 19.1 Wazabuni wana haki ya kuomba mapitio ya maamuzi ya mchakato wa Ununuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwenye anuani ya taasisi nunuzi au Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (PPAA) na nakala ya malalamiko itumwe PPRA kwenye anuani zifuatazo: |

| | |
|---|---|
| | Anuani ya PPAA:<br><br>Katibu Mtendaji,<br>Mamlaka ya Rufaa za Zabuni,<br>S. L. P 9310,<br>**DAR ES SALAAM**<br><br>Anuani ya PPRA kwa ajili ya Nakala:<br><br>Afisa Mtendaji Mkuu,<br>Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma,<br>Jengo la Kambarage,<br>Ghorofa ya 9,<br>Barabara ya PSPF,<br>S. L. P 2865,<br>**41104 DODOMA.** |

# HATI MAHSUSI YA MAMLAKA YA KIAPO CHA KISHERIA

## HATI MAHSUSI YA MAMLAKA YA KIAPO CHA KISHERIA

**KWA WOTE WANAOHUSIKA**

KWA Hati hii ya Mamlaka ya Kisheria iliyotolewa tarehe ***31/12/2021***

Sisi ambao saini zetu zimeoneshwa hapa chini ***MASHANI CONSTRUCTION AND GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED wa S.L.P 1098 TANGA,*** kwa mamlaka tuliyopewa ya azimio ya Bodi ya Wakurugenzi Na. *08* ya tarehe 30 mwezi 12 mwaka 2021

Tunamteua na kumuidhinisha Ndugu ***SHABANI ALLY MRINDOKO*** kuwa mwakalishi wetu halali kisheria akiwa na mamlaka kamili kwa niaba yetu na kwa majina yetu na kwa maslahi na faida yetu kufanya moja au yote kati ya haya yafuatayo katika kutekeleza Zabuni Na **ME /007/2021-22/RRHTAN/W/10**; Hii ikimaanisha kufanya jambo lolote kwa niaba ya kampuni na kufanya jambo lolote linalohusiana na Zabuni Na **ME /007/2021-22/RRHTAN/W/10** inayohusu **UKARABATI WA CHUMBA CHA ICU** kwa ya taasisi **HOSPITALI YA RUFAA MKOA TANGA.**

**NA KWAMBA** hati hii sanifu ya nguvu ya kisheria haitabatilisha au kuathiri hati sanifu yoyote ya mamlaka ya kisheria itakayotolewa kwa mtu yeyote au watu wengine wowote kwa mamlaka ya aina hiyo na kwamba mamlaka hayo yatabaki kuwa na nguvu na mamlaka kana kwamba hati hii haijatolewa.

**NA KWAMBA** tunaidhinisha kitu chochote ambacho mwakilishi wetu, wakala au mbadala wake atakayemteua kwa mamlaka yake atakachokifanya kwa mamlaka yake katika kutekeleza au kukusudia kutekeleza kwa kuzingatia mamlaka ya hati hii sanifu ya nguvu ya kisheria.

Imewekwa lakiri ya kamapuni **MASHANI CONSTRUCTON AND GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED** mbele yetu leo hii tarehe 30 mwezi 12 mwaka 2021

**KWA USHUHUDA** makubaliano haya yamesainiwa leo tarehe 30 mwezi 12 mwaka 2021 hapa TANGA kwa niaba ya **MASHANI CONSTRUCTION AND GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED**

Imewekwa lakiri na kutolewa hapa **TANGA na Mashani Construction And General Supplies Co. LTD**

Ambaye ninamfahamu /ametambulishwa **N/A**

Ambaye nimemfahamu leo tarehe ***31/12/2021***

Pahmadhani
..........................
**MTOA IDHINI**

**MBELE YANGU:**

**Jina:** PHILEMON RAULENCIO

**Saini:** ..............................

**Wadhifa:** ADVOCATE

PHILEMON RAULENCIO ADVOCATE Notary Public & Commissioner for Oaths P O BOX 1895 TANGA

Imesainiwa na kupokelewa hapa TANGA

**SHABANI ALLY MRINDOKO**

ambaye ninamfahamu /ametambulishwa na **N/A**

ambaye nimemfahamu leo tarehe ***31/12/2021***

..........................
**MPOKEA IDHINI**

**MBELE YANGU:**

**Jina:** PHILEMON RAULENCIO

**Saini:** ..............................

**Wadhifa:** ADVOCATE

PHILEMON RAULENCIO ADVOCATE Notary Public & Commissioner for Oaths P O BOX 1895 TANGA

## AHADI YA MTOA HUDUMA KUHUSU SERA DHIDI YA RUSHWA, KANUNI ZA MAADILI NA PROGRAMU YA UKIDHI

Kampuni hii **MASHANI CONSTRUCTION AND GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED** tunaweka umuhimu katika zabuni ya ushindani unaofanyika kwa misingi ya haki na huru na isiyoruhusu unyanyasaji. Tunapenda kuthibitisha kuwa hatutatoa wala kuwezesha moja kwa moja au siyo moja kwa moja ushawishi usiofaa au zawadi kwa afisa yeyote wa umma, ndugu zake au watu wenye uhusiano wa kibiashara, kuhusiana na kotesheni hii au baadaye katika utekelezaji wa mkataba kama tutafanikiwa.

Kampuni hii, ina Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukidhi inayojumuisha hatua zote za maana na muhimu kuhakikisha kuwa ahadi yetu ya kutotoa rushwa iliyotolewa katika maelezo haya itazingatiwa na menejimenti yetu na waajiriwa na pia watu wengine wote wanaofanya kazi nasisi katika miradi ya sekta ya umma au mkataba ikiwa ni pamoja na wakala, washauri, wabia wetu na watoa huduma wetu wasaidizi. Nakala zetu za Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya Ukidhi zimeambatishwa.

ABUBAKARI RAMADHANI

*(Jina la mtu aliyepewa mamlaka)*

*Sahihi*

31/12/2021

*Tarehe*

MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES CO. LTD. P.O. Box 1098 TANGA TANZANIA

*Muhuri/ Alama ya Kampuni*

1. **Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni**

*Tarehe 31/12/2021*

**M/S** *MASHANI CONSTRUCTION AND GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED*

Kwa: *MGANGA MFAWIDHI,*
*HOSPIALI YA RUFAA MKOA TANGA,*
*S.L.P 452,*
***TANGA***

Baada ya kupitia Nyaraka za Zabuni pamoja na nyongeza yake [*N/A*, Sisi, tunaahidi kutekeleza kazi ya **UKARABATI WA CHUMBA CHA ICU, ME/007/2021-22/RRHTAN/W/10** kulingana na Nyaraka za Zabuni hii kwa jumla ya Bei ya Mkataba ya ***[MILIONI KUMI NA TATU NA SABINI ELFU NA MIA MBILI HAMSINI TU, 13,070,250/=]*** Shilingi za Tanzania au kwa jumla ya bei itakayobainishwa kulingana na Jedwali la Bei lililoambatanishwa kama sehemu ya Zabuni hii.

Tuna afiki uteuzi wa **NATIONAL CONSTRUCTION COUNCIL OF TANZANIA (NCC)** kuwa Msuluhishi wetu katika migogoro yoyote itakayojitokeza wakati wa Mkataba.

Au

Hatuafiki uteuzi wa kuwa Msuluhishi, na tunampendekeza **[*N/A*]** kama mbadala wake, ambaye ada yake kwa siku na sifa zake zimeambatanishwa.

Kama Zabuni yetu itakubaliwa, tuko tayari kutekeleza kazi ya ujenzi kwa mujibu wa mpango wa kazi uliowasilisha.

Endapo, Zabuni yetu itakubaliwa, tuko tayari kuwasilisha Tamko la Dhamana ya Utekelezaji Kazi kama lilivyoanishwa kwenye Nyaraka za Zabuni.

Tunatamka kwamba bei ya Kotesheni yetu haitokani na makubaliano na Wazabuni wengine kwa lengo la kuvuruga/kuharibu mchakato. Aidha, hatujawasilisha zabuni zaidi ya moja kwenye mchakato huu.

Tunathibitisha kwamba tunakubaliana na kipindi cha uhai wa zabuni kilichoainishwa katika Kifungu cha 7 cha Maelekezo Mahsusi kwa Wazabuni na tunakubali kufungwa na masharti ya Zabuni hii kwa kipindi chote kabla ya mwisho wa uhai wa Zabuni.

Pia tunaahidi kukamilisha kazi iliyotajwa katika kipindi cha **siku thelathini (30)** ambacho kinajumuisha kipindi cha maandalizi.

Kotesheni hii pamoja na barua yako ya kukubali kwa maandishi vitafanya mkataba baada ya kusainiwa kwa Mkataba. Tunafahamu kuwa haulazimiki kukubali kiwango cha chini au kotesheni yoyote kati ya kotesheni unazopokea.

Tunathibitisha kuwa kotesheni hii imetimiza masharti kama yanavyotajwa katika Mwaliko wa Kotesheni.

Saini Idhinishwa: Ramadhani (ABUBAKARI RAMADHANI)

Jina na Cheo cha Mweka Saini: PROJECT MANAGER AND COORDINATOR

Jina la Mzabuni: MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIER

MASHANI CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES CO. LTD.
P.O. Box 1098
TANGA
TANZANIA

## 2. Tamko la Dhamana ya Zabuni

Tarehe: *31/12/2021*

Namba ya Zabuni: ***ME/007/2021-22/RRHTAN/W/10***

Namba Mbadala: ***[N/A]***

Kwa: *MGANGA MFAWIDHI*

*HOSPITALI YA RUFAA MKOA TANGA,*

*S.L.P 452,*

***TANGA.***

Tunatoa tamko kuwa:

Tunafahamu kwamba, kulingana na masharti yako, Zabuni hii lazima iwasilishwe na Tamko la Dhamana ya Zabuni.

Tunakubali kuwa, tutazuiliwa kushiriki katika michakato ununuzi wa umma katika kipindi cha muda utakaobainishwa na Mamlaka, kama tutavunja majukumu yetu yaliyopo katika masharti ya zabuni, kama:

(a) Tutaondoa au kubadilisha Zabuni yetu ndani ya muda wa Uhai wa Zabuni ulioainishwa katika Fomu ya Zabuni;

(b) Tutapingana na masahihisho ya kihesabu yalifanyika katika bei ya Zabuni; au

(c) Tutajulishwa juu ya kukubali kwa Zabuni yetu na TN katika kipindi cha Muda wa Uhai wa Zabuni na kushindwa kutekelezwa yafuatayo:

  i. Kushindwa kusaini mkataba pale itakapotakiwa na TN;

  ii. Kushindwa au kukataa kutoa Dhamana ya Utendaji Kazi au kukidhi masharti mengine yanayoendana na usainishaji wa mkataba kama ilivyobainishwa katika Nyaraka za Zabuni.

Tunafahamu kuwa, Tamko hili la Dhamana ya Zabuni litaisha muda wake kama hatutokuwa Mzabuni mshindi, pale (i) tunapopokea taarifa ya mzabuni aliyeshinda zabuni; au (ii) siku ishirini na nane (28) baada ya ukomo wa mwisho wa Zabuni yetu.

Saini: ........................................

Katika uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji

Jina: ***SHABANI ALLY MRINDOKO***

Aliyeidhinishwa kusaini Zabuni kwa niaba **ya *MASHANI CONSTRUCTION AND GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED***

Tarehe 31/12/2021

Muhuri wa Kampuni (inapofaa)

MASHANI CONSTRUCTION
P.O.Box 1098
TANGA
TANZANIA
& GENERAL SUPPLIES CO. LTD.

# SCHEDULE OF MATERIALS

| ICU REHABILITATION - BOMBO RRH | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | UNIT | QTY | PRICE-TZS | AMOUNT |
| | | | | | |
| A | <u>MATERIALS</u> | | | | |
| | | | | | |
| 1 | **WALLING** | | | | |
| | Blocks | Pcs | 600 | 1,450 | 870,000 |
| | Sand | Trips | 2 | 130,000 | 260,000 |
| | Cement-50kgs | Bags | 30 | 15,000 | 450,000 |
| | | | | | |
| 2 | **PAINTING & DECORATION** | | | | |
| | Emulsion Paint - 20 LTRS | bckt | 5 | 35,000 | 175,000 |
| | wall putty | bags | 7 | 25,000 | 175,000 |
| | Emulsion Paint for wall putty mixing | bckt | 4 | 35,000 | 140,000 |
| | Latex primer (Binder) | bckt | 4 | 85,000 | 340,000 |
| | Silk paint 20ltr | bckt | 6 | 145,000 | 870,000 |
| | Weather G paint 20ltr | bckt | 4 | 145,000 | 580,000 |
| | Sand paper no. 120 | m | 5 | 2,000 | 10,000 |
| | Brush 2''Tz | pc | 5 | 1,500 | 7,500 |
| | Solvent - 5LTRS | TIN | 2 | 25,000 | 50,000 |
| | Roller 9'' | Pcs | 5 | 5,000 | 25,000 |
| | | | | | |
| 3 | **DOORS** | | | | |
| | Door shutter | Pcs | 2 | 450,000 | 900,000 |
| | Door frame | Pcs | 2 | 220,000 | 440,000 |
| | Iron mongery | Pcs | 2 | 70,000 | 140,000 |
| | Door hinges 4' | pair | 3 | 15,000 | 45,000 |
| | | | | | |
| 4 | **ALUMINIUM PARTITION** | | | | |
| | Aluminium works | item | 1 | 16,000,000 | 16,000,000 |
| | | | | | |
| 5 | **ELECTRICAL WORK** | | | | |
| | Electrical rehabilitation + Backup Gen. | Item | 1 | 67,550,000 | 67,550,000 |
| | | | | | |
| 6 | **ICT WORKS** | Item | 1 | 25,000,000 | 25,000,000 |
| | | | | | |
| 7 | **OXYGEN INSTALLATION WORKS** | Item | 1 | 18,000,000 | 18,000,000 |
| | | | | | |
| 8 | **PLUMBING WORKS** | Item | 1 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| | | | | | |
| 9 | **OVERHEADS** | | | | |
| | Water bill | Item | 1 | 150,000 | 150,000 |
| | Electricity bill | Item | 1 | 300,000 | 300,000 |
| | Transport | Item | 1 | 2,100,000 | 2,100,000 |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | **TOTAL COST OF MATERIALS** | | | | **144,577,500** |

# SCHEDULE OF LABOUR'S